# Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili

***Said A. M. Khamis***
Chuo Kikuu cha Bayreuth

Neno vionjo linatumika kwa uwili wa maana hapa. Kwanza, hali ya kimajaribio au mwondoko wa utanzu fulani wa fasihi kutoka sura iliyozoeleka kwendea sura mpya inayoanza kujishikashika. Hali ya umajimaji inayotoa sifa bainifu fulani, lakini isiyo na mgando bado, na kwa hivyo kutoweza kuitwa mtindo kwa maana ya trend kwa Kiingereza. Pili, maana ya kuirambisha na kuionyesha hadhira kwa 'viishira' kukisia wapi riwaya mpya ya Kiswahili inalekea.

Mara moja tunaona neno vionjo liinajisemea lenyewe kimyakimya juu ya mabadiliko ya utanzu wa fasihi. Ni kawaida kwamba utanzu wa fasihi hupata mtekenyo wa mabadiliko ili kuepuka kupooza na kushindwa kushawishi kwa fikra na umbuji. Kanuni muhimu hapa ni kwamba hatimaye, chenye mwanzo kina mwisho – sharti kichoke, lazima kipoteze nguvu na msisimko wake. Kwa mfano – mabadiliko ya ushairi wa Kiswahili ya kutotii sheria kali za arudhi na badala yake kunogea miundo huru, inasemekana, angalau kwa baadhi ya washairi na wasomi, ni kutokana na kupooza kwa sulubu zake za ndani, mbali na sababu nyingine za nje. Lakini kwa upande mwingine, utanzu wa fasihi, bila ya kuchoka au kupooza, huweza ukajikuta ghafla kutoweza kuhimili nguvu za matukio muhimu ya kihistoria, kitamaduni, kijamii, kisiasa, kielimu na hata kiuchumi – nguvu zinazolazimisha kubadilika kwake kifani na kimaudhui.

Tukichukua mfano mwingine, mabadiliko ya riwaya ya ramsia huko Ulaya, kuelekea riwaya ya uhalisia ya akina Defoe, Richardson na Fielding, inakubalika kwamba yalitokea kwa taathira zilizochangiwa na mapinduzi ya viwanda. Na mabadiliko hayo yasichukuliwe kwa kubadilika kwa mifumo ya kiuchumi tu, bali mwenendo mzima wa maisha ya watu wa huko, ikiwemo nyenzo za mauzo na manunuzi, usambazaji bidhaa, uhusiano wa mtu na mtu, kufa kwa fikra zilizoonekana kongwe pamoja na fikra za kuuangusha Uungu zilizozushwa na wasomi kama Nietzsche, na hatimaye kukua na kupata nguvu kwa ubinafsi na utashi wa vitu. Tusisahau pia namna gani, vita vya kwanza na vya pili vya dunia na matokeo yake ya kukatisha tamaa, yalivyopelekea kuzaliwa katika sanaa, usasa *(modernism)* na tena usasabaadaye *(postmodernism)*. Arnold Kettle (1959: 30 – 31) anaitetea hoja hii:

> Mapinduzi makubwa katika jamii za watu hubadilisha urazini; na si kupindua husiano zao za kijamii tu, bali pia mitazamo, falsafa na sanaa zao … (tafsiri yangu).

Fasihi ya Kiswahili nchini Kenya na Tanzania pia haikuepuka kuelemewa na matukio makuu nje ya miundo ya tanzu zake. Kwa mfano, nchini Kenya waandishi wa fasihi ya Kiswahili wanaoandika kwa misimamo wazi ya kisiasa hawajai kiganja tele. Kinyume chake, nchini Tanzania, tukitoa wale wanaoandika riwaya pendwa, ambazo kwa hakika nyingi zikichunguzwa zinasema mambo fulani ya kisiasa, wote wanajishughulisha, moja kwa moja, na siasa katika kazi zao za tanzu mbalimbali. Sababu zilizopelekea tofauti hizi ziko wazi. Makali ya wembe ya siasa za Kenya dhidi ya siasa za kisoshalisti yalikuwa kila wakati yako tayari kumkata mwandishi aliyekataa kutetea mfumo wa kiuchumi wenye misingi ya kibepari. Kwa upande wa Tanzania, waandishi, kwa namna moja au nyingine, waliathiriwa na Azimio la Arusha na siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Hapa pia haikuwa rahisi kuandika dhidi ya sera rasmi. Hali zote hizi ziliweka bila ya kutamka, kanuni za kuandika kazi za sanaa ambazo ziliwahakikishia wasanii urahisi wa kufuata mkondo wa kanuni hizo bila ya kuingiliwa. Hii haina maana kwamba hakukuwa na waandishi waliozivunja kuta za makatazo na vizuizi. Kwa mfano, kwa upande mmoja tuliona *Ngojera za Ukuta* za M. E. Mnyampala (1970) na mkusanyo wa *Mashairi ya Azimio la Arusha* wa G. Kamenju na F. Topan (1974), ulivyoimba nyimbo za Azimio la Arusha. Na kwa upande mwingine, tumeshuhudia *Mashetani* (1971) ya E. Hussein, *Gamba la Nyoka* (1979) ya E. Kezilahabi, *Njozi Iliyopotea* (1980) ya C. G. M. Mung'ong'o na *Nyota ya Huzuni* (1981), ya G. Liwenga, zilivyokataa kuimba kikasuku nyimbo za aina hiyo. Lakini hata kule kutofuata mkondo wa kisiasa na kanuni za uandishi zilizoteuliwa na tabaka tawala, kulimaanisha kunaswa katika mkondo huo pia. Kwa mfano kauli ya Kezilahabi katika *Gamba la Nyoka* (1978: 150) haiwezi kujinasua kufuata hali hii kwa sababu lengo lake ni kujibu na kwenda kinyume na mawazo na sheria zilizotawala wakati ule:

> Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa mzee Cholongo na wengine wa aina yake. Jamii ilikuwa imemwacha nyuma. Jamii ilikuwa imejinyumbua na sasa haikuwa pale alipokuwa. Ukale una wakati wake. Ukale unastahili kuchunguzwa, lakini haudumu milele […] Naam, hivyo ndivyo Tanzania ilivyojengwa, hivyo ndivyo ilivyojiendeleza na ndivyo ilivyojinyumbua. Kulikuwa na watu waliopenda kweli Ujamaa, nao walikuwa na sababu zao. Kulikuwa na watu walioupinga, nao walikuwa na sababu zao. Kulikuwa na wanampinduzi na wapinga mapinduzi na kulikuwa na wanafiki.

Majaribio na mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili yalianza pale waandishi wengi wa Kenya na Tanzania, walipoanza kukataa kuitikia 'hewalla' kwa kila walichokiona na kukisikia. Pia walipokataa kuitikia kanuni na pingamizi za ubunaji na sanaa walizozikuta au walizowekewa. Mwanzoni, njia bora iliyoonekana ingefaa kutumika katika kazi za fasihi ni ile ya uhalisia, kwa sababu ya uwazi na mnyooko

wake wa mantiki. Pia kwa sababu uhalisia ni mwelekeo au mtindo uliozoewa sana, si Afrika Mashariki na Afrika nzima tu, bali duniani kote. Ni mbinu iliyoota mizizi imara kwa muda mrefu. Na isitoshe, kwa sababu ya uwazi na kutobabaisha kwake, ilionekana ni njia bora kabisa ya kufichua na kuueleza umma matatizo ya kijamii na kisiasa kinagaubaga. Ilisemekana kwamba ilikuwa njia bora ya kuwasiliana na wananchi, hasa wananchi wa kawaida. Na kusema kweli, uhalisia wenyewe kwa wakati huu ulikuwa haujaondoka katika misingi ya uwazi na mantiki. Matakwa ya wananchi na matakwa ya nchi yaliyokuwa yakizungumzwa na wanasiasa yalikuwa bado hayajabainika kuwa ndoto tupu. Yalikuwa na uhalisia wa aina fulani. Na hata yalipoonekana kuwa ni ndoto, ilidhaniwa si vibaya kuota. Jambo la kusisitizwa hapa ni kwamba katika hali zote hizi za nchi mbili, uhuru wa mwandishi kwa namna moja au nyingine, ulikabwa kimyakimya bila ya kutangazwa, ikawa kama ni sehemu ya kubanwa kwa aina nyingi nyingine za uhuru wa wananchi.

Lakini, tokea kuanza kuvuma upepo wa mageuzi, inaonekana kwamba waandishi wamepata mwanya mkubwa zaidi wa uhuru wa kisanaa na kifikra. Sasa midomo mingi inaisemea siasa badala ya mdomo mmoja au michache, ingawa mara nyingi bila ya taathira kubwa. Nadhani dalili za uhuru huo ziko wazi katika hii riwaya mpya tunayoisemea kama itakavyodhihirika katika vionjo hivi.

Lakini ni lazima tuseme kwamba, mbali na kuathiriwa kimabadiliko ndani na nje ya miundo ya utanzu wenyewe, utanzu wa riwaya kwa kawaida ni regerege na tepetepe, wenye kugeukageuka na kubadilika. Hauna mashiko hata hivyo kimuundo na kifikra. Katika kitabu chao *The Nature of Narrative*, R. Scholes na R. Kellogg (1968) wanaungama kwamba riwaya ni mchanganyiko usio na mashiko thabiti, mchanganyiko wa ubunifu na usayansi, wa ramsia na ngano kwa upande mmoja, na kwa upande wa pili, wa historia na uigaji. Bergonzi (1972: 15) analijumlisha jambo hilo kwa msemo wake maarufu kuwa riwaya haina tena upya.

Dalili za upya wa riwaya ninayoizungumzia, zimo katika usanii na maudhui yake. Kisanaa kuna mabadiliko mengi ya kushangaza na kutatiza: muundo na vitomeo vyake vya fani na umbuji katika mbinu inayojaribu kuasi kwa makusudi uhalisia mkongwe, uhalisia mkavu. Mbinu ya fantasia inajitokeza katika kila kipengele cha riwaya hii mpya: usimulizi, uhusika, mwingiliano wa wahusika, mwanya wa kisaikolojia ndani ya vichwa vyao, ndoto zinazoingiliana na ukweli wa mambo, matukio katika mshikamano wa uzoefu na ugeni wa mambo, mazingira na jinsi yanavyoshikana na matukio na kufungamana na wahusika kihistoria, umataifa, usayansi na mabaki ya uchawi, ushirikina na mazingaombwe; na hatimaye

mwingilianomatini *(intertextuality)* na mchezo wa lugha, kupelekea wakati mwingine hata kuingia katika ugo wa kimetafizikia.

Mbinu hizi zinakubaliana na kwenda bega kwa bega kabisa na maudhui mapya. Kusema kweli, huu ni wakati mzuri kwa uandishi wa riwaya, wakati ambao waandishi wamepata upeo mkubwa sana wa kufaidi vituko na miujiza. Milango mingi imefunguliwa. Utandawazi umeota mizizi. Malaika wameshoneka midomo na mbawa zao zimedumka. Mashetani wanaingia wapendavyo hata misikitini na makanisani. Kinyume na zamani, mashetani wanatoa mioto midomoni mwao bila ya kizuizi. Watu wamekanyagika na kubabapaa kiuchumi, sawasawa na mikeka mibovu inayokanyagwa. Wamenyang'anywa utu wao na kwa hivyo wanaweza kufanya lolote, hata kununuliwa bila ya kuhisi aibu au fedheha. Tamaa ya nafuu au kupona haipo. Hofu imetawala. Hujui leo kuna nini, sikwambii kesho. Sheria hazisimami tena. Fahamu zimetutoka. Hatukumbuki ya jana seuze ya juzi. Kwa upande mmoja, jeuri zimezidi na kwa upande mwingine unyonge umeteremka daraja ya chini kabisa uliokowahi kufikia. Tunatazamana, lakini hatuonani wala hatujuani – hatuoneani huruma tena. Soma magazeti, sikiliza redio. Kuna lugha ambazo zamani hatujapata kuzisikia. Watu wanachunwa ngozi. Vibaka. Mama kazaa kitoto njiani na kukitupa mtaroni. Wizi umekithiri hata miongoni mwa wale wanaolinda mali ya raia isiibiwe. Ufisadi ndio mtindo wa kisasa. Uasharati ndio pumzi zetu, hatuwezi kulala bila ya kuonja. Binti anakula chungu kimoja na mama yake. Mume kambigija mke na kumwua. Pigapiga. Vunjavunja. Mtu huona, husikia au hukutwa na mambo ambayo miaka kumi iliyopita yasingemkuta. Chambilecho P. Roth (1982: 33) katika makala yake ya "Writing American Fiction":

> …(haya ni) mambo ambayo yanatujaza ajabu, mshangao na woga, pia na maradhi na kukata tamaa. Majungu, kashfa na kasheshe, kichaa, upumbavu, usalihina wa uwongo, kelele … ni vitu vilivyomo katika ukweli na ndoto wakati mmoja…na nguvu za kubadilisha karne hii, kubadilisha maisha yangu na yako, kwa hakika hazimo katika chombo chochote kile … (tafsiri yangu).

Kimaudhui, riwaya hii mpya ina mtazamo wa kuyaona matatizo yetu kwa msisitizo wa ndani zaidi kuliko nje. Nje inachukuliwa kuwa ni pembejeo tu la matatizo yote. Wakati mwengine, baadhi ya watunzi wa riwaya hii hujitoa kwa kiasi fulani katika kushughulikia matatizo ya ndani ya nchi na kutazama matatizo ya kidunia na kimataifa. Pengine haya yalishughulikiwa kwa kiasi na wanariwaya wa Kiswahili hapo zamani, lakini si kwa msisitizo na vuguvugu hili la sasa. Katika mifano yote ya riwaya hii mpya, unaziona na kuzisikia hasira kali za waandishi wake ambao

wana tamaa kwamba watawakoleza wasomaji wao woga na hasira, wanapoikumbusha hadhira kitisho wanachokijua.

Kifani uandishi wa aina huu, hasa kwa kiasi fulani katika mwegemeo wake wa fantasia, ulianza kuonekana katika riwaya za Shaaban Robert: *Kusadikika* (1951) *Adili na Nduguze* (1952), *Kufikirika* (1967), *Siku ya Watenzi Wote* (1968) na *Utubora Mkulima* (1968). Na pia katika miaka ya 1960 na 1970 katika tamthilia za E. Hussein, *Kinjeketile* (1969), *Mashetani* (1971) na baadaye *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (1976). Pia katika hadithi fupi ya S. A. Mohamed, *Mjadala Kwenye Kiburuji* (1971), hadithi fupi ya M. S. Mohamed, *Mateso (*1974), thamthilia za S. A. Mohamed, *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Amezidi* (1995); thamthilia ya E. Mbogo, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na riwaya yake ya *Vipuli vya Figo* (1996) na hadithi fupi na riwaya kadhaa za E. Kezilahabi, zikiwemo *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975).

Kifani na kimaudhui katika upya huu tunaozungumzia hapa, waandishi watano wamejitokeza zaidi. Nao ni E. Kezilahabi na *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1990), Katama Mkangi na *Walenisi* (1995), E. Mbogo na *Vipuli vya Figo* (1996), W.E. Mkufya na *Ziraili na Zirani* (1999), S. A. Mohamed katika *Babu Alipofufuka* (2001), na K. W. Wamitila na *Bin-Adamu* (2002).

Hapa basi, tuingie ndani kwa ufafanuzi wa vipengele vya kisanaa na kimaudhui vya riwaya hii mpya kwa kukita katika vionjo vya riwaya ya *Nagona* tu, riwaya ambayo kwa namna moja au nyengine, ni kiwakilisho kizuri cha riwaya hii mpya. Tuanze na usimulizi.

Ingawa mbinu za usimulizi wa waandishi hawa zinatofautiana miongoni mwao na baina ya riwaya na riwaya za mwandishi mmoja, kwa jumla tunaweza kusema simulizi zao zinaonyesha tabia ya kukwepa mtiririko wa moja kwa moja na sahili wenye kufuata mantiki. Ni simulizi zenye kuoanisha sauti mbalimbali katika mchangamano mkubwa usioshikana kabisa na mantiki ya wakati na pahala kama hadhira zetu zilivyozoea. Njia kuu ya usimulizi wa *Nagona* kwa mfano, ni ile ya kuyamwaga na kufufuliza matukio, mawazo, falsafa na siasa ya mwandishi na kuyaacha yashikamane na mtiririko wa hadithi bila ya kiungo bayana cha ploti kupitia visababisho na athari za visababisho katika mtiririko wa wakati na mahali. Matokeo ya mpiko huu wa mawazo ya falsafa, siasa na matukio ya hadithi yanayofululiza, ndiyo hatimaye yanayokuwa kiini cha maudhui ya riwaya hii.

Mawazo kwa mzo, yanayogusa kila kipengele cha jamii ya ki-Afrika na pia matatizo ya kimataifa, yanasimuliwa vipandevipande na kuachwa yaelee tu hewani. Msimulizi mkuu ni 'mimi', mhusika mkuu, lakini hapa na pale, wahusika wengine wanaingia na kutoka harakaharaka wakionekana na kusikika kwa muda mfupi. Hapa simulizi ya hadithi inaruhusiwa ipige hatua. Pale maelezo ya kifalsafa yanaachwa yatawale. Tena mawazo ya kidini yanafuatia. Baadaye siasa inaingia. Hivyohivyo tokea mwanzo mpaka mwisho. Mkufu unaofungamanisha mawazo na simulizi na kufunganisha matukio na matendo unaungwa kiufundi kabisa. Ni mkufu wa kipengele cha safari, isiyojulikana mwanzo wala mwisho wake. Safari ya kumtafuta Mwokozi wa Pili ambaye anatazamiwa kuuokoa ulimwengu na balaa. Mwisho wa hadithi au simulizi, kama ungaliweza kuitwa mwisho, uko wazi. Si ule wa hadithi za mtindo wa kihalisia ambapo mara nyingi huwa na kikomo fulani. Hivi hapa vionjo vya simulizi hii:

**Usimulizi wa nafsi ya kwanza wa safari ya mhusika mkuu**

> … Yaelekea ilikuwa jioni, maana kulikuwa na mwanga hafifu wa kidhahabu humo bondeni nilimokuwa. Sikumbukii kuona jua na sikumbukii kuona mtu mwengine karibu nami … Kama huo ulikuwa mwanzo wa safari yangu, sina hakika. Lakini nilijikuta nimechoka (1) …

**Falsafa**

> ...Uwaonao katika duara hii ni kikundi kidogo tu cha waliokuwa wabishi katika usakaji wa njia. Yule pale ni Plato, na yule ni Socrates. Huyu ni hapa ni Aristotle. Yule ni Hegel, huyu ni Darwin na waliokaribiana nawe ni Marx na Freud na huyu ni Nietzsche (15) …

**Siasa**

> … Nchi yetu ilikuwa imekumbwa na janga la njaa. Nchi nyingi katika ulimwengu wa tatu zilipata pigo kubwa na mamilioni ya watu walikufa. Migogoro mingi ya kiuchumi iliendelea kuisakama dunia (18) …

**Safari kwa mara nyingine tena ikiashiriwa na sauti isiyojulikana ya nani**

> … Chukua uta na mshale kutoka hilo jiwe bapa karibu nawe. Tangu sasa wewe ni mfwasi mkuu wa kitoto kilichozaliwa (62 - ukurasa wa mwisho)…

Sauti ambayo inatawala katika *Nagona* ni ya mimi ambayo inasimulia hadithi ya safari ambamo mimi anakutana na wahusika wengine, na kuathiriwa na vitu anavyoviona na matukio mbalimbali yanayotokea. Ni mhusika mjuayote, ingawa katika riwaya hii, mara nyingi haingii vichwani mwa watu. Mfululizo wa simulizi na hadithi unafanywa mgumu kwa kugeuzika wakati mara kwa mara. Na kile kinachoufanya usimulizi wa *Nagona* uwe mgumu zaidi ni kukutanishwa kwa sauti za watu na sauti za vitu mbalimbali ambazo zinakuja kama mawimbi ya bahari

iliyochafuka, na tena sauti hizo zote zikikamatana na metonimia, sitiari, ishara na picha mbalimbali, sentensi baada ya sentensi, ukurasa baada ya ukurasa, kuifanya matini nzima ya riwaya kuwa ngumu kueleweka kimaana. Sauti ya mto unaolindwa na nyoka, sauti za miguu ya mtu nyuma ya mimi, sauti za ndege, sauti za vikohozi, sauti za miti inayocheka, sauti za watu wanaosoma kwa njia mbalimbali na kwa mparaganyiko. Fikiria mchanganyiko wa sauti hizi za wanadamu, wanyama na vitu kwenye ukurasa mmoja, sauti zinazozuka kwa ajabu na miujiza. Hii hapa sauti ya mimi kwa mfano, ikidhihirisha sauti nyingine:

> Kama huo ulikuwa mwanzo wa safari yangu, sina hakika. Lakini nilijikuta nimechoka. Mbele yangu, niliona jiwe moja jeusi. Nilijikokota kwenda kulikalia. Kabla sijakaa nilisikia mtu akikohoa. Kwa hofu, nilisimama wima, nikaangalia huku na huko. Hapakuwa na mtu! Nilipokuwa bado nashangaa nilisikia nyayo za mtu akitembea nyuma yangu. Nilishtuka. Nyuma sikuona mtu. Nilikuwa wapi hapa! Nilitembea kwa harakaharaka kutoka hapo mahali. Nilianza kusikia sauti za watu wasomao vitabu. Walikuwa wakisoma bila ya kusikilizana. Kila mmoja alikuwa akisoma lake. Sikuona watu wala shule … Kichomi kilianza kuniuma ubavuni. Nilipiga magoti chini. Kwa maumivu nilianza kutembelea magoti. Nilisikia vicheko karibu katika kila mti. Msitu mzima ulianza kunicheka. Niliona matawi ya miti yakianza kuchezacheza kwa upepo. Ghafla miti yote iliacha kucheza na vicheko vikaisha. Kukawa shwari.

Mbinu nyingine muhimu ya *Nagona* na ambayo pia inajitokeza katika riwaya mbili mpya za S. A. Mohamed ni ile ya **mwigilianomatini** – jambo ambalo linaufanya muundo wa riwaya hii kuwa wa kigeugeu. Kezilahabi mara kwa mara anaazima dhana za kivisaasili za ki-Afrika, visaasili vyenyewe, ploti na ngano za kifasihisimulizi. Hizi anazipiganisha na vitomeo vya falsafa za Kimagharibi, ishara na picha za Ukristo na Uislamu, similizi za miungu ya ki-Giriki pamoja na kile anachokifinyanga kwa ubunifu wake yeye mwenyewe. Kwa mfano, ili *mimi* aweze kutekeleza lengo la kumpata Mwokozi wa Pili, lazima amnase paa wa kichawi kwanza. Usakaji wake wa paa huyo unaelezwa katika simulizi ya ki-Afrika ambapo mhusika mbabe anavishinda vikwazo vinne: msitu, jangwa, mto na mlima na halafu anayamudu matakwa magumu ya mfalme katika utekelezaji wake huo. Mambo mengi ya ajabu na miujiza yanatokea katika simulizi inayoegemea mbinu inayoitwa *uhalisiamazingaombwe* ambamo Yesu na Muhammad wanafufuliwa na kuhuishwa.

*Nagona* pia, kama riwaya za Mkangi na Mohamed, inatumia mkarara na marudiorudio kama inavyothibitishwa kwa mfululizo mkubwa wa maneno na vikundi vya maneno vinavyofanya kazi ya kisitiari, ishara na 'vitajwa' *(allusions)*. Katika mfululizo na mkarara, maneno kama ukweli, mshumaa, vichaa, vicheko, ungamo kuu, ukimya, njia, barabara, mto, paa, ndege, mti (miti), msitu, milima,

mabonde, duara, vitabu, ukosefu wa watu, paka, mkombozi, ajali, ndoto, maluweluwe, uta, na mshale, yanafanya kazi ya kutilia mkazo dhamira, mapuuza, uharibifu wa mazingira, unyonyaji, upumbavu, unafiki, vifo na falsafa za urasimu.

Uwazi wa mwanzo na mwisho wa riwaya ni kipengele muhimu cha riwaya hii ambacho pia kinajitokeza katika riwaya ya Mohamed, *Babu Alipofufuka*. Katika *Nagona,* mwanzo ni wa kushtukia tu. Kusema kweli huku kushtukia katika riwaya hii ni kwa kuambukiza – kunajitokeza tena na tena. Huu hapa mwanzo wa simulizi ya Nagona :

> Yaelekea ilikuwa jioni, maana kulikuwa na mwanga hafifu wa kiadhabu humo bondeni nilimokuwa. Sikumbukii kuona jua na sikumbukii kuona mtu mwingine jaribu nami …

Mwanzo wa riwaya hii hauhusiani na wakati na pahala maalum, lakini ni kituo cha nukta ya duara. Na hata mbele katika simulizi dhana ya wakati na mwahala huganda kabisa. Mwisho ni mwanzo katika dhana ya safari, kwa sababu *mimi* anapewa tena kazi ya safari ya utafutaji kitu. Paa aliyenaswa kakimbia na Mkombozi wa Pili hajathibitika hasa. Katika aya ya mwisho mimi anatumwa tena (62):

> Chukua uta na mshale kutoka hilo jiwe bapa karibu nawe …

Kipengele kingine kinachobainisha mwondoko wa riwaya ya Kiswahili kuelekea upya ni kipengele cha uhusika. Katika *Nagona* mhusiku mkuu ni wa kivisaasili na kitenzi. Ni muhusika anayetawala riwaya yote. Mbali na kazi aliyopewa na mwandishi kumtafuta paa wa kichawi ili hatimaye akutane na Mwokozi wa Pili ana kazi ya kuisimulia na kwenda na hadithi yenyewe kimatendo, kimatukio, kiwakati na kimahali. Kupitia maneno yake na vitendo vyake tunaonyeshwa na kujuvywa mengi kuhusu wahusika wengine, fikra na mawazo na mikinzano ya kifalsafa, dini na siasa. Kupitia kwake pia, ama kwa usimulizi au vitendo au vituko mbalimbali, tunaonyeshwa kuporomoka kwa jamii zetu na maafa yanayoelekea kuikumba dunia nzima. *Mimi* si mhusika wa mwili na roho, na kwa hivyo mwandishi haonyeshi hamu yoyote ya kumchora sura, wasifu na tabia zake. Ni kivuli tu, ambacho kinatumiwa na mwandishi kama chombo cha kuwasilishia mawazo yake na chombo cha kuisukuma mbele hadithi. Pamoja na wahusika wengine, hakuna hata mara moja ambapo tunaona ufunuzi wa saikolojia yao, au motisha ya visababisho na matokeo au mtanzo wa mwingiliano baina yao. Kila mhusika ni sehemu tu ya kusaidia kukamilisha lengo la mwandishi la kutolea mawazo yake na kukamilisha simulizi ya safari. Katika kufanikisha dhima hii, wahusika wamepewa hata nguvu za kichawi na miujiza. Wanaweza kuondosha

milima na kumeza maji yote ya mto na kuyatema tena na kunyoosha mguu kwa maelfu ya maili kuchukua kitu. Na kama nilivyosema, *mimi* hana nyama wala mifupa – mhusika asiye na ugandifu kabisa, aliyewahi kuumbwa katika fasihi ya Kiswahili.

Baadhi ya wahusika wengine wanaonyeshwa kuwa hai au bora tuseme, hawajafa. Wengine, mitume na manabii (Yesu na Muhammad) au wanafalsafa akina Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Darwin, Marx, Freud na Nietzsche tunajua wameshakufa, lakini katika riwaya hii wanafufuliwa. Wakati mwingine wanakosa mno vitambulisho hata hujui nani ni nani, kama vile mhusika fulani anapoungama (uk. 47) msomaji anakuwa hana hakika kama anayeungama ni mimi au nani.

Lugha inayotumika katika *Nagona* ni wazi, angavu na rahisi, ukichukulia kwa kipimo cha maneno yaliyotumika. Lakini riwaya nzima ni ngumu kueleweka kwa sababu kadha. Kwanza, kwa upana wa mwanya wa ulinganisho baina ya kilinganishi na kinacholinganishwa. Na si hivyo tu, picha anazozichora mwandishi zinatoka nje ya mantiki na uzoefu wa wasomaji wake. Hakuna ukaribu wa ulinganishi. Pili, lugha ya *Nagona,* inatonewa mfululuizo wa picha za *uhalisiamazingaombwe,* ajabu na miujiza. Msomaji hapati nafasi ya kupumua na kushusha pumzi kabla hajafumwa na ajabu na miujiza mingine. Tatu, katika mfuatilio wa sentensi moja kukamatanishwa na nyingine, kuna upotevu wa vifungo vya uhusiano wa kimaana. Nne kuna ukosefu wa visababisho vya matokeo.

Tena katika riwaya hii tunayoiita mpya, kuna hali ya kupotosha kwa makusudi muundo, sura au umbo la riwaya ya uhalisia tunayoijua kwa kupunguza au kuingiza vitu (k.m. nambari, picha, orodha, harufi yombo, harufimkozo, n.k.) au kuingiza vitu ambavyo kwa kawaida haviketi katika mwili wa riwaya tulizozizoea. Katika *Nagona* mambo matatu yanafanyika: sura ya nane yote imeandikwa kitamthilia tu, kwa mfuatilio wa mazungumzo pande mbili; na sura ya kumi (sura ya mwisho) ina ukurasa mmoja tu (ukurasa 62) ambao una aya nne. Na mwisho, riwaya yenyewe ni riwaya fupi (kurasa 62 tu), lakini ina uchangamano unaoifanya kuwa ngumu kimuundo na kimaana.

Kimaudhui, *Nagona* ina mikondo miwili. Mkondo wa kutazama maisha ya kimwetu na mkondo wa kujishughulisha na matatizo ya kimataifa. Mara kwa mara, hasa mwanzomwanzo, tunaonyeshwa uoza ambao tumeuzoea na kuujua vizuri. Tunaonyeshwa hivyo kwa picha zinazorejelewa tena na tena. Kutawala kwa ukimya na hofu. Watu hawasemi ingawa unawaona katika madhila. Watu

wanakufa bila ya kuzikwa. Paka ndio waliobaki na wanaonekana kuwa na uamuzi juu ya watu. Vitabu ni adui mkubwa na kwa hivyo vinaachwa vizongwe na mavumbi na kuoza. Hakuna maji kila pahala. Maovu ya karne nne yameyageuza maji kuwa damu. Hakuna anayeshangaa au kuungama au kusema chochote isipokuwa *mimi* na mzee mmoja. Hali hii inafikia upeo sura ya nane ambapo kuna ungamo la uoza na maovu (47 – 49):

> Ningependa kuungama dhambi zifuatazo: Nimezini mara nyingi … (Mwanamke) mmoja mchana na usiku mmoja … Nimeshiriki katika mauaji ya watu wanne … Niliwapa fedha watu fulani waniulie hao watu … Niliiba pesa za umma …

Hali hii, kwa kiwango fulani inaelezwa katika riwaya hii kuwa inasababishwa na ushirikiano wa nguvu za ndani na kutoka nje (18 – 19):

> Nchi yetu ilikuwa imekumbwa na janga la njaa. Nchi nyingi katika ulimwengu wa tatu zilipata pigo kubwa na mamilioni ya watu walikufa. Migogoro mingi ya kiuchumi iliendelea kuisakama dunia … Ghafla harufu mbaya iliingia puani mwetu …]Oh! Mmefanya vizuri kunikumbusha. Karibu nisahau. Pua zangu zimeshazoea mambo haya … Njooni nitawaonyesha matokeo ya hasira. Njiani tulianza kuona vinyesi vimepangwa kandokando ya njia, vikavu na vibichi … Hakuna haja ya kuwafikisha mbali. Humu mwote ni mahali walipozikwa wafalme wa Uingereza, Ureno, watawala wa Ufaransa na maraisi wa Marekani. Palikuwa mahali panapoheshimiwa sana. Lakini vichaa fulani waishio katika bonde lile huja kujisiadia …

Katika kiwango hikihiki, Kezilahabi anachora picha mbili muhimu anazoziita (katika tasnifu yake ya udaktari, 1985) *quassia* au *tonicum*. Picha moja inahusiana na raha ya kutapika roho yake mtu; hali ambayo inazua maumivu makali kifuani na kitovuni. Hii ni njia pekee, kwa mujibu wa mwandishi, ya kusafisha na kuweza kuiona roho yake mtu ni safi. Picha nyingine ni ya ngoma kuu ambayo inadhihirika kuchezwa mwishoni mwa riwaya hii, ambapo katika mashindano, ngoma ya wendawazimu inatia fora kushinda ngoma nyingine zilizochezwa na watu wakubwa, wenye elimu na kujua mambo (59).

> Tuliendelea kucheza kwa vurumai […] Sote tulikuwa tumechoka. Vichomi vimekwishatupata. Wengi wetu tulikuwa tumeshikilia mbavu kwa maumivu, lakini kwa shida tuliendelea kucheza.

Hapa Kezilahabi anaonekana kusema kuwa maendeleo ya nchi zetu za ki-Afrika yatapatikana tu kwa kutochelea maumivu na hali ngumu sana – la muhimu ni kucheza ngoma yetu wenyewe badala ya kuiga ngoma za watu wengine.

Katika kiwango cha kimataifa, *Nagona* inaonekana kujishughulisha na matatizo kama yale ya uchafuzi wa mazingira au kuhusu mwanya unaozidi kutanuka baina ya nchi tajiri na nchi za kimasikini au tishio la vita vya silaha za maangamizo. Katika hali zote mbili za matatizo ya ndani na ya kimataifa, Kezilahabi anasisitiza hatari ya unafiki na mzubao wa kufwata viongozi kama vipofu. Kufwata ndoto ya mtu mwenye vichwa vingi na tena kufuata kwa uchangamfu na kutojali nini kinatokea hata kama kuna uharibifu na kurudi nyuma:

> Hao watu wamekufa au wazima? […] Kama kufa ni kutokuwako basi wazima. Zaidi ya hayo maisha tuyajuayo yaweza kuwa ndoto za mtu mmoja mwenye vichwa vingi …

Riwaya ya *Nagona* ni kiwakiliso cha riwaya mpya inayoanza kujishika na kujiimarisha kutokana na utepetepe wake. Ni riwaya ambayo ndiyo kwanza inachimbuka na kwa hivyo inatafuta sifa zake bainifu na hatimaye kukubalika. Ni riwaya ya siku zijazo – riwaya inayokimbia vilazimisho au kanuni zilizowekwa na jamii. Ni kielelezo cha vipi waandishi wake wanavyofikiri juu ya uhuru wa sanaa na uhuru wa mawazo. Ni riwaya ya waandishi wenyewe, si riwaya ya baadhi ya watu katika jamii wanavyotaka iwe. Inadhihirika hivyo kifikra, kimuundo na kisanaa. Msingi wake mkubwa ni kutumia fantasia ili kuondoa uchovu na uzoefu wa kiumbuji uliopo. Inafanya hivyo kwa kusomba mbinu za kiutunzi za ki-Afrika (hasa kutokana na hazina ya fasihi simulizi) na mbinu za kimataifa, (k.m. *uhalisiamazingaombwe* ambao ni maarufu Amerika ya Kusini, ingawa si mgeni Afrika) na kujaribu mbinu za kuvuka usasa, kuingia usasabaadaye. Ingawa mielekeo ya kutumia mbinu hizi kama itakavyoonekana siku za usoni, ni tofauti baina ya mwandishi na mwandishi na baina ya kazi na kazi ya mwandishi mmoja, lengo ni kutumia fantasia kufinyangia kero na hasira za waandishi kuhusu nchi zetu zinavyoangamia.

## Marejeo


Bergonzi, B. (1972), *The Situation of the Novel*, Penguin, London.
Bertoncini, E. (1989), *Outline of Swahili Literature (Prose, Fiction and Drama)*, E. J. Brill, Leiden
Brooks, D. (1991), *Modernism – Encyclopedia of Literature and Criticism*, (eds), Coyle, et al, routledge, London.
Foster, E. M. (1974), *Aspects of the Novel*, Penguin, London.
Gromov, M. D. (1998), *Nagona and Mzingile: Novel, Tale or Parable – Swahili Forum* V, AAP, No. 55, Institut für Afrikanistik, Universität Köln, Köln.
Harrow, K. W. (1994), *Thresholds of Change in African Literature – The Emergence of Tradition – Studies in African Literature,* Heinemann Portsmouth and James Currey, London.
Hussein, E. (1969), *Kinjeketile*, Oxford University Press, Nairobi.
Hussein, E. (1971), *Mashetani*, Oxford University Press, Nairobi.
Hussein, E. (1976), *Jogoo Kijijini na Ngao za Jadi*, Oxford University Press.
Kamenju, G. & topan, F. (1974), *Mashairi ya Azimio la Arusha*, Longman Tanzania, Dar-eds-Salaam.
Kettle, A. (1959), *An Introduction to the English Novel*, Vol. 1, Hutchinson University Library, London.
Kezilahabi, E. (1974), *Kichwamaji*, East African Publishing House, Dar-es-Salaam.
Kezilahabi, E. (1975), *Dunia Uwanja wa Fujo*, East African Literature Bureau, Dar-es-Salaam.
Kezilahabi, E. (1975), *Gamba la Nyoka*, Eastern Africa Publication, Arusha.
Kezilahabi, E. (1985), *African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation*, (Ph.D thesis), University of Wisconsin-Madison.
Kezilahabi, E. (1990), *Nagona*, Dar-es-Salaam University Press, Dar-es-Salaam.
Liwenga, G. (1981), *Nyota ya Huzuni*, Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam.
Mbogo, E. (1988), *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, Education Services Centre Ltd, Dar-es-Salaam.
Mbogo, E. (1996), *Vipuli vya Figo*, East African Educational Publishers, Nairobi.
Mkangi, K. (1995), *Walenisi*, East African Educational Publishers, Nairobi.
Mkufya, W.E. (1999). *Ziraili na Zirani*, Hekima Publishers, Dar-es-salaam.
Mnyampala, M. (1970), *Ngonjera za Ukuta*, Kitabu cha Kwanza, Oxford University Press, Dar-es-Salaam.
Mohamed, S. A. (1988), *Pungwa*, Longman Kenya, Nairobi.
Mohamed, S. A. (1990), *Kivuli Kinaishi*, Oxford University Press, Nairobi.
Mohamed, S. A. (1996), *Amezidi*, Oxford University Press, East African Educational Publishers, Nairobi.
Mohamed, S. A. (2001), *Babu Alipofufuka* (kitatoka karibuni), The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi, Nairobi.
Mohamed, S. A. (2003), *Dunia Yao* (mswada)

Mohamed, S. M. (1974), *Mateso – Mapenzi ni Kikohozi; Hekaya za Kuburudisha*, Longman, Nairobi.
Mulokozi, M. M. (1982), *Protest and Resistance in Swahili Poetry 1660 – 1885 – Kiswahili*, tol. 49/1, Machi, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam.
Mulukozi, M. M. (1975), *Revolution and Reaction in Swahili Poetry – Kiswahili*, tol. 45/2 Septemba, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam.
Mung'ong'o, C. G. (1980), *Njozi Iliyopotea*, Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam.
Nietzsche, F. (1969), *Thus Spoke Zarathustra*, Penguin, London.
Nietzsche, F. (1984), *Human, All Too Human,* Penguin, London.
Nietzsche, F. (1990), *Beyond Good and Evil*, Penguin, London.
Roth, P. (1982), *Writing American Fiction – The Novel Today*, Fontana Paperbacks, Glasgow.
Salami, M. (1992), *John Fowle's Fiction and the Poetics of Postmodernism,* Fairleigh Dickinson University Press, London.
Scholes, R. & Kellogg, R. (1968), *The Nature of Structure*, Oxford University Press, London.
Wamitila, K.W. (2002). *Bina-Adamu*, Phoenix Publishers, Nairobi.
Watt, I. (1976), *The Rise of the Novel*, Penguin, London.